ULENIN

AU

UBEBERU WA KISOSHAL?

Kwa Ajili ya Uadhimisho wa
Mwaka wa Mia Tokea Kuzaliwa Lenin
Mtukufu

OFISI YA UCHAPAJI WA LUGHA ZA KIGENI
PEKING

LUC

ULENIN

AU

UBEBERU WA KISOSHAL?

Kwa Ajili ya Uadhimisho wa
Mwaka wa Mia Tokea Kuzaliwa Lenin
Mtukufu

Imeandikwa
na Idara za Wahariri wa Magazeti ya
Renmin Ribao, Hongqi na
Jiefangjun Bao

(Aprili 22, 1970)

OFISI YA UCHAPAJI WA LUGHA ZA KIGENI
PEKING 1970

Kimepigwa chapa katika Jamhuri ya Watu wa China

Vladimir Ilyich Lenin,
Mwalimu Mkubwa wa Mapinduzi ya Kifanyakazi.

Ulenin ni Umarx katika zama za ubeberu na za mapinduzi ya kifanyakazi.

Stalin: "Msingi wa Ulenin"

YALIYOMO

1. Bendera ya Ulenin Haishindiki 1

2. Udikteta wa Kifanyakazi ni Suala la Msingi la Ulenin 8

3. Upinduzi wa Serikali wa Kipinga Mapinduzi wa Kikundi cha Mahaini cha Khrushchov-Brezhnev 12

4. Usoshalisti Midomoni, Ubeberu Vitendoni 28

5. Ule Uitwao "Ubrezhnev" ni Udhalimu Halisi 38

6. Ndoto ya Urivishenisti wa Soviet Juu ya Milki Kubwa 49

7. Watu wa Dunia Nzima, Unganeni na Piganeni Kwa Ajili ya Kuuangusha Ubeberu wa Kimarekani, Urivishenisti wa Soviet na Wapinga Maendeleo wa Nchi Mbali Mbali 64

1. BENDERA YA ULENIN HAISHINDIKI

Uadhimisho wa utimiaji miaka mia tokea kuzaliwa Lenin mtukufu umeangukia tarehe 22 Aprili mwaka huu.

Wafuasi wa Umarx-lenin, tabaka la kifanyakazi na watu wa kimapinduzi wa dunia nzima, wakiwa na heshima kubwa kabisa juu ya Lenin mtukufu, wanaiadhimisha siku hiyo yenye maana ya kihistoria.

Baada ya Marx na Engels kufariki dunia, Lenin akawa kiongozi mtukufu wa vugu vugu la ukoministi la ulimwengu na mwalimu mtukufu wa tabaka la kifanyakazi na watu wote wanaokandamizwa wa dunia nzima.

Katika 1871, mwaka wa pili wa kuzaliwa Lenin, ulitokea mwinuko wa

Commune ya Paris, nao ulikuwa ni jaribio la kwanza lililofanywa na tabaka la kifanyakazi kulipindua tabaka la kibepari. Mwishoni mwa karne ya 19 na mwanzoni mwa karne ya 20, Lenin alipoanza shughuli zake za kimapinduzi, ilikuwa ndipo dunia ikiingia katika zama za ubeberu na za mapinduzi ya kifanyakazi. Katika mapigano ya kuupinga ubeberu, uopotyunisti wa aina mbali mbali, na hususan kuupinga urivishenisti wa *International* ya Pili, Lenin aliurithi, aliuhami na aliukuza Umarx na kuuinua juu kufikilia daraja mpya — daraja ya Ulenin. Kama Stalin alivyosema, **"Ulenin ni Umarx katika zama za ubeberu na za mapinduzi ya kifanyakazi."**[1]

Lenin alichambua hitilafu za ubeberu, alifichua kanuni zinazouendesha ubeberu na alitanzua mkururo wa masuala muhimu kuhusu mapinduzi ya kifanyakazi katika zama za ubeberu pamoja na suala kuhusu kuwa usoshalisti **"utapata**

ushindi kwanza katika nchi moja au nchi kadha”.[2] Alifanya ufafanuzi juu ya fikra ya kuwa tabaka la kifanyakazi lazima likamate madaraka ya uongozi katika mapinduzi ya demokrasi ya kibepari, na aliliongoza tabaka la kifanyakazi la Urusi kufanya mazoezi makuu — mapinduzi ya mwaka 1905. Mapinduzi Makuu ya Oktoba ya Kisoshalisti yaliyoongozwa naye yalileta mabadiliko ya msingi kutoka dunia kongwe ya kibepari hadi dunia mpya ya kisoshalisti, na kufungua zama mpya za historia ya binadamu.

Lenin alitoa michango mikubwa mno kwa jihadi ya mapinduzi ya kifanyakazi katika upande wa nadharia na matendo.

Baada ya Lenin kufariki dunia, Stalin aliirithi na aliihami jihadi ya Ulenin katika mapigano ya kupinga maadui wa kitabaka wa nchini na wa nje na kuwapinga waopotyunisti wa Kulia na wa “Kushoto” ndani ya Chama. Stalin

aliwaongoza watu wa Soviet Union kuendelea kusonga mbele kwenye njia ya kisoshalisti na kupata ushindi mkubwa. Katika Vita vya Pili vya Dunia, watu wa Soviet Union, wakiongozwa na Stalin, wakawa nguvu kuu katika kuushindia ushambulizi wa ufashisti na walitoa michango mikubwa na adhimu ambayo itadumu milele katika historia ya binadamu.

Wakoministi wa China na watu wa China daima hatutosahau kwamba ndio kutokana na Ulenin, tuliigundua njia yetu ya ukombozi. Komredi Mao Tsetung alisema: **"Mlio wa mizinga wa Mapinduzi ya Oktoba ulituletea Umarx-lenin." "Machina waliugundua Umarx-lenin, ukweli unaofaa po pote duniani, na sura ya China ikaanza kubadilika."**[3] Komredi Mao Tsetung aliainisha: **"Watu wa China daima wanayachukua mapinduzi ya China kuwa ni maendelezo ya Mapinduzi Makuu ya Oktoba ya Kisoshalisti".**[4]

Kwa kutumia nadharia ya Umarx-lenin, Komredi Mao Tsetung alitanzua kwa busara masuala ya msingi ya mapinduzi ya China na aliwaongoza watu wa China kufanya mapigano ya kimapinduzi na vita vya kimapinduzi vya muda mrefu kabisa, vikali kabisa, vigumu kabisa na vyenye mazonge mazonge mengi kabisa katika historia ya mapinduzi ya kifanyakazi ya ulimwengu na kupata ushindi wa mapinduzi ya umma katika China, nchi hii kubwa ya Mashariki. Huu ni ushindi mkubwa kabisa uliopatikana katika mapinduzi ya kifanyakazi ya ulimwengu baada ya Mapinduzi ya Oktoba.

Hivi sasa, tumo katika zama mpya tukufu za mapinduzi ya ulimwengu. Ikilinganishwa na ile ya wakati wa Lenin alipokuwa yu hai, hali ya ulimwengu imetokewa na mabadiliko makubwa ya kuitikisa dunia. Ukuaji wa historia ya ulimwengu mzima umehakikisha usahihi wa nadharia ya kimapin-

duzi ya Lenin na umethibitisha kuwa bendera ya Ulenin haishindiki.

Lakini, historia ina vilima na mabonde yake. Kama ulivyotokea urivishenisti wa Bernstein-Kautsky baada ya Engels kufariki dunia, vile vile umetokea urivishenisti wa Khrushchov-Brezhnev baada ya kifo cha Stalin.

Baada ya miaka 11 tangu Khrushchov kushika utawala, mafarikiano yalitokea miongoni mwa urivishenisti, Brezhnev akachukua mwahala pa Khrushchov, naye keshapitisha miaka mitano na kitu, na sasa katika Soviet Union ni mtu kama huyu ndiye amechukua uwenyekiti katika "kuadhimisha" siku ya kutimia miaka mia tangu kuzaliwa Lenin.

Lenin aliwahi kusema: **"Katika historia mara kwa mara hutokea hali kama hii: Baada ya kufariki dunia tu wale viongozi wa kimapinduzi wanaojulikana kwa sifa zao miongoni mwa matabaka yanayokandamizwa, mara**

maadui zao hujaribu kuiba majina yao ili kuyadanganya matabaka yanayokandamizwa."[5]

Hivyo ndivyo hasa haini Brezhnev na wenzake wanavyomtendea Lenin mtukufu. Katika ule ati wauitao *Muhtasari wa Uadhimisho wa Siku ya Kutimia Miaka Mia Tangu Kuzaliwa Vladimir Ilyich Lenin*, bila ya kujali cho chote, wamepotosha kimachomacho sura adhimu ya Lenin, mwalimu wa kimapinduzi wa tabaka la kifanyakazi, na kufanya mambo yao ya uwongo ya kirivishenisti kuwa kama ni Ulenin. Wanajidai "kumuadhimisha" Lenin, lakini kwa kweli wanaiba jina la Lenin kuharakisha kutekeleza ubeberu wa kisoshal, ufashisti wa kisoshal na umilitaristi wa kisoshal. Hayo ni matusi makubwa kabisa kwa Lenin!

Kufedhehi vilivyo uhaini uliofanywa na mahaini wa urivishenisti wa Soviet juu ya Ulenin, kufichua tabia ya kitabaka ya ubeberu wa kisoshal wa

urivishenisti wa Soviet, kudhihirisha mwendo wa kisheria wa kihistoria wa kuangamia bila ya muepuko wo wote kwa ubeberu wa kisoshal kama ubeberu wa kibepari na kuzidi kuyasukuma mbele mapigano makubwa ya watu wa dunia ya kupinga ubeberu wa Kimarekani, urivishenisti wa Soviet na wapinga maendeleo wa nchi mbali mbali, hayo ndiyo majukumu yetu ya kimapigano ya hivi sasa. Na hapa ndipo ilipo maana kubwa ya maadhimisho yetu kwa siku ya kutimia miaka mia tangu kuzaliwa Lenin mtukufu.

2. UDIKTETA WA KIFANYAKAZI NI SUALA LA MSINGI LA ULENIN

Katika mapigano yake ya kupinga uopotyunisti na urivishenisti, Lenin alifahamisha tena na tena kwamba suala la msingi la mapinduzi ya kifanyakazi ni kunyakua hatamu za kiserikali

kwa nguvu, kuvunjilia mbali mashine ya dola ya kibepari na kuanzisha udikteta wa kifanyakazi.

Lenin alisema: Dola ya kibepari **"haiwezi kuchukuliwa mwahala pake na dola ya kifanyakazi (udikteta wa kifanyakazi) kwa njia ya 'kunyauka'; kwa mujibu wa kanuni ya kawaida, haya yanawezekana kwa njia ya mapinduzi ya nguvu tu."**[6]

Lenin aliengeza: Nadharia ya Marx kuhusu udikteta wa kifanyakazi **"ina mahusiano yake yasiyotengeka na nadharia yake yote kuhusu kazi za kimapinduzi za tabaka la kifanyakazi katika historia. Na udikteta wa kifanyakazi ndiyo mwisho wa kazi hizo".**[7]

Ushindi wa Mapinduzi ya Oktoba yaliyoongozwa na Lenin ndio ushindi wa nadharia ya Umarx kuhusu mapinduzi ya kifanyakazi na udikteta wa kifanyakazi. Njia ya Mapinduzi ya Oktoba ndiyo njia ya tabaka la kifanyakazi kujinyakulia udikteta wa kifanya-

kazi kwa kupitia mapinduzi ya kutumia nguvu.

Kabla na baada ya kutokea Mapinduzi ya Oktoba, Lenin alijumlisha matendo mepya ya kimapinduzi, na aliikuza zaidi nadharia ya Umarx kuhusu udikteta wa kifanyakazi. Alidhihirisha: Mapinduzi ya kisoshalisti **"ni zama nzima iliyojaa mapambano makali ya kitabaka"**,[8] **"madhali zama hii haijamalizika, basi bila ya shaka wanyonyaji damu wataendelea kuwa na tamaa ya urejeshwaji na kuigeuza tamaa hiyo kuwa majaribio ya urejeshwaji"**.[9] Ndiyo kwa maana hiyo, Lenin alichukulia kwamba udikteta wa kifanyakazi **"ni wa lazima . . . si kwa tabaka la kifanyakazi lililokuwa limeshalipindua tabaka la kibepari tu, bali vile vile kwa zama nzima ya kihistoria kati ya ubepari na 'jamii isiyo na tabaka' yaani ukoministi"**.[10]

Leo, tunapoadhimisha siku ya kutimia miaka mia tangu kuzaliwa Lenin,

iko maana kubwa kabisa kwa hivi sasa kudurusu tena fikra hizo adhimu za Lenin.

Kama kila mmoja ajuavyo, ni katika suala hili hili la msingi kuhusu mapinduzi ya kifanyakazi na udikteta wa kifanyakazi, ndiyo kikundi cha mahaini warivishenisti wa Soviet kimeuhini Ulenin na Mapinduzi ya Oktoba.

Hapo mapema, wakati sura ya urivishenisti wa Khrushchov ilipokuwa ikifichuka tu, Komredi Mao Tsetung mara akadhihirisha kwa ukali: **"Naona zipo 'panga' mbili: Mmoja ni Lenin na mwengine ni Stalin. Sasa upanga huu Stalin umetupwa na Warusi." "Ama upanga huu Lenin, jee, tunaweza kusema kama sasa pia umetupwa kwa kiasi fulani na baadhi ya viongozi wa Soviet Union? Nionavyo mimi, wameutupa kwa kiasi cha kutosha. Mapinduzi ya Oktoba bado yanafaa? Bado yanaweza kuwa mfano kwa nchi mbali mbali? Ripoti ya Khrushchov kwenye Mkutano**

Mkuu wa 20 wa Wajumbe wa Chama cha Kikoministi cha Soviet Union ilisema kuwa inawezekana kupata hatamu za kiserikali kwa kupitia njia ya bunge, hii ndiyo kusema kwamba imekuwa si lazima kwa nchi mbali mbali kujifunza kwa Mapinduzi ya Oktoba. Wakati mlango huu ulipofunguliwa tu, mara Ulenin ukatupiliwa mbali kwa jumla."[11]

3. UPINDUZI WA SERIKALI WA KIPINGA MAPINDUZI WA KIKUNDI CHA MAHAINI CHA KHRUSHCHOV-BREZHNEV

Ilikuwaje urejeshwaji ubepari umetokea katika Soviet Union, nchi ya kisoshalisti ya kwanza ulimwenguni, na ilikuwaje ikawa ubeberu wa kisoshal? Kama tukiyachungua masuala haya kwa mtizamo wa Umarx-lenin, hususan kwa nadharia ya Komredi Mao Tsetung kuhusu kuendelea na mapinduzi chini

ya udikteta wa kifanyakazi, tutaweza kuelewa kwamba hii hasa ni aina moja ya zao la mapigano ya kitabaka nchini mwa Soviet Union, ni tokeo la kuwa mamlaka ya Chama na dola yamenyakuliwa na kijikundi cha wachukua njia ya kibepari wenye mamlaka katika Chama cha Soviet, yaani tokeo la hatamu za kiserikali za tabaka la kifanyakazi kunyakuliwa na tabaka la kibepari la Soviet Union. Kwa wakati huo huo, ni tokeo la siasa ya "mabadiliko ya amani" ambalo ubeberu wa kilimwengu, kwa ajili ya kujiokoa kutoka kwenye uangamiaji wake, umeiteke leza katika Soviet Union kwa kupitia kikundi cha mahaini warivishenisti wa Soviet.

Komredi Mao Tsetung amedhihirisha: **"Jamii ya kisoshalisti ni kipindi kirefu cha kutosha cha kihistoria. Katika kipindi hichi cha kihistoria cha kisoshalisti, bado yapo matabaka, hitilafu za kitabaka na mapigano ya kitabaka, bado**

yapo mapigano baina ya njia ya kisoshalisti na ya kibepari, na bado ipo hatari ya urejeshwaji ubepari."[12]

Mapigano ya kitabaka katika jamii ya kisoshalisti bado yanakutanika juu ya suala la hatamu za kiserikali. Komredi Mao Tsetung amedhihirisha: **"Wale wawakilishaji wa tabaka la kibepari waliojipenyeza ndani ya Chama, serikali, jeshi na sehemu mbali mbali za utamaduni ni kikundi cha warivishenisti wa kipinga mapinduzi. Hali ikishaiva tu, watanyakua hatamu za kiserikali na kuugeuza udikteta wa kifanyakazi kuwa udikteta wa kibepari."**[13]

Matabaka na mapigano ya kitabaka yameendelea kuwepo siku zote katika Soviet Union baada ya Mapinduzi ya Oktoba ingawa tabaka la kibepari lilipinduliwa. Stalin aliwahi kulitoa kundi kubwa sana la wawakilishaji wa tabaka la kibepari wa kipinga mapinduzi waliojipenyeza ndani ya Chama, kama Trotsky, Zinoviev, Kamenev, Radek,

Bukharin, Rykov na wenzao. Haya yamethibitisha kwamba mapigano ya kitabaka siku zote yalikuwa yakiendelea kwa vikali na kwamba siku zote iliikuwepo hatari ya urejeshwaji ubepari.

Kwa kuwa Soviet Union ilikuwa ni dola ya kwanza ya udikteta wa kifanyakazi, kwa hivyo ilikuwa haina maarifa ya kutosha juu ya suala la namna gani kuuimarisha udikteta wa kifanyakazi na kuepukana na urejeshwaji ubepari. Katika hali ya namna hiyo na baada ya Stalin kufariki dunia, Khrushchov, mchukua njia ya kibepari mwenye mamlaka aliyekuwa akijificha katika Chama cha Kikoministi cha Soviet Union, kwa njia ya hujma ya ghafla alitoa "ripoti ya siri" ya kumzulia Stalin kwa uovu, na akitumia aina zote za mbinu za uovu na za kijanja, alinyakua mamlaka ya Chama na dola katika Soviet Union. Huu ulikuwa upinduzi wa serikali wa kipinga mapinduzi ambao umeugeuza udikteta wa kifanyakazi

kuwa udikteta wa kibepari, na ambao umeupindua usoshalisti na kuurejesha ubepari.

Brezhnev alikuwa mshiriki wa Khrushchov katika upinduzi wa serikali wa kipinga mapinduzi, na baadaye akachukua mahala pa Khrushchov. Kushika utawala kwake, kwa kiini, ni maendelezo ya upinduzi wa serikali wa kipinga mapinduzi wa Khrushchov. Brezhnev ni Khrushchov wa Pili.

Komredi Mao Tsetung amedhihirisha: **"Kushika utawala kwa urivishenisti ndiyo kushika utawala kwa tabaka la kibepari."[14] "Soviet Union ya leo, inatekeleza udikteta wa kibepari, udikteta wa tabaka la mabepari wakubwa, udikteta wa aina ya ufashisti wa Ujerumani, udikteta wa aina ya Kihitler."[15]**

Hoja yenye busara ya Komredi Mao Tsetung imefafanua kwa kina kirefu mno tabia hasa ya kitabaka na asili ya kijamii ya ubeberu wa kisoshal wa

urivishenisti wa Soviet na imeainisha tabia yake ya kifashisti.

Baada ya kikundi cha mahaini warivishenisti wa Soviet kunyakua mamlaka ya Chama na dola katika Soviet Union, daraja yenye fursa maalum ya tabaka la mabepari la Soviet imepanua sana sana mamlaka yao ya kisiasa na ya kiuchumi; imechukua nyadhifa za utawala katika Chama, serikali, jeshi na mambo ya uchumi na utamaduni; tena kutoka ndani ya daraja hiyo, limeumbika tabaka la mabepari mabwana-serikali wenye kuhodhi — tabaka la mabepari wakubwa la aina mpya, ambalo limetawala mashine yote ya dola na kudhibiti utajiri wa jamii nzima.

Tabaka hilo la mabepari mabwana-serikali wenye kuhodhi la aina mpya, kwa kutegemea hatamu za kiserikali walizozidhibiti, limegeuza mpango wa umilikiaji wa kisoshalisti kuwa mpango wa umilikiaji wa wachukua njia ya kibepari na kubadili uchumi wa kisosha-

listi kuwa uchumi wa kibepari na uchumi wa ubepari wenye kuhodhi wa dola. Kwa jina la "dola", linaiba hazina ya dola kiwazimu na kwa kutumia mbinu za kila aina limepokonya kama lipen-

davyo matunda ya jasho ya watu wa Soviet, na linastarehea maisha ya anasa na ya uasherati na linafanya ujeuri na kiburi juu ya umma.

Tabaka hilo la mabepari mabwana-serikali wenye kuhodhi la aina mpya ni tabaka la kibepari ambalo limegeuza **tamaa ya urejeshwaji** kuwa **majaribio ya urejeshwaji.** Nalo liliwakandamiza wana mashujaa wa Mapinduzi ya Oktoba, likapanda juu ya vichwa vya watu wa makabila mbali mbali ya Soviet Union na limejenga kijibaraza chao cha ufalme cha kipinga mapinduzi. Kwa hivyo, linapinga kabisa maendeleo, linawachukia kabisa na kuwaogopa kabisa umma.

Kama matabaka yote ya kipinga maendeleo yaliyodidimia, tabaka hilo la

mabepari mabwana-serikali wenye kuhodhi la aina mpya limejaa hitilafu za kila aina ndani yake. Kwa ajili ya kuhifadhi kwa ukomo wa nguvu zao mamlaka waliyoyanyakua, huwa wanashirikiana kimbwa na kinguruwe na huku wakipikiana majungu na kupingana. Kila shida zao zikizidi, mchuano wao wa hadharani na faraghani huzidi kuwa mkali zaidi.

Ili kukamua faida kwa kiwango kikubwa kabisa na kuhifadhi utawala wao wa kipinga maendeleo, tabaka hilo la mabepari mabwana-serikali wenye kuhodhi la aina mpya si kama linawanyonya damu na kuwakandamiza wananchi wa nchini mwao wenyewe tu, bali pia bila ya mwepuko wo wote linafanya ushambulizi na upanuzi wa ardhi wa kiwazimu, linajiunga katika safu la ubeberu wa kilimwengu katika kuigawa dunia na kuendeleza siasa ovu kabisa ya ubeberu wa kisoshal.

Tabaka hilo la mabepari mabwana-serikali wenye kuhodhi la aina mpya ni msingi wa kitabaka wa ubeberu wa kisoshal wa urivishenisti wa Soviet. Sasa, mwakilishaji mkuu wa tabaka hilo ndiye Brezhnev. Naye kwa kiwazimu ameutekeleza, na ameukuza urivishenisti wa Khrushchov na yumo katika kukamilisha mabadiliko kutoka urejeshwaji ubepari hadi ubeberu wa kisoshal ambayo yalikuwa yameshaanzishwa katika wakati wa utawala wa Khrushchov.

Baada ya Brezhnev kushika utawala, ameeneza ati "utaratibu mpya wa uchumi" katika kila upande na kuweka kanuni ya faida ya kibepari katika sheria, hivyo amezidisha unyonyaji damu wa maoligaki wa mabwana-serikali wenye kuhodhi juu ya watu waishio kwa jasho lao. Bila ya kujali umma kufa au kupona, akina Brezhnev wanawatoza kodi kwa kishenzi na kutekeleza siasa ya Hitler ya "mizinga badala ya siagi", na

wanaharakisha uenezi wa mambo ya kijeshi katika uchumi wa kitaifa ili kuambatana na mahitajio ya ubeberu wa kisoshal katika kufanya upanuzi wa kijeshi na matayarisho ya kivita.

Ilivyokuwa kikundi cha mahaini warivishenisti wa Soviet kinakwenda kinyume kwa ukaidi, kwa hivyo kimeleta uharibifu mkubwa kabisa katika nguvu za prodakshen za kijamii na kuleta matokeo ya hatari sana. Kazi za viwanda zimeanguka, kilimo kimeshuka chini, mifugo imepungua, pengo kati ya utoaji wa manoti na bidhaa limezidi, utoaji vitu umekuwa wa wasi wasi, bidhaa zimeadimika ajabu katika masoko ya dola, na watu waishio kwa jasho lao wanafukarika zaidi siku hata siku. Mahaini warivishenisti wa Soviet si kama wamefuja idadi kubwa ya fedha iliyorundikwa na watu wa Soviet Union kwa kazi za bidii za makumi ya miaka tu, bali vile vile wamejidhalilisha kwa kuomba mikopo kwa Ujerumani

ya Magharibi — nchi iliyoshindwa katika Vita vya Pili vya Dunia, hata wamefika hadi kuuza utajiri wa maumbile wa nchi na kuzishawishi rasilmali zenye kuhodhi za Japani kuingia katika Siberia. Uchumi wa Soviet Union wa siku hizi umejitumbukiza katika msukosuko usiotanzulika. Tukiwa ni marafiki wa watu wa Soviet Union, sisi watu wa China na watu wa dunia tunaona ghadhabu kubwa isiyo na kifani juu ya mahaini warivishenisti wa Soviet ambao wameleta maafa na aibu ya namna hii katika maskani ya Ulenin; na tunaonyesha hurúma zetu nyingi za kidhati kwa umma mkubwa wa watu wa Soviet ambao wanateswa kwa machungu mengi katika hali ya utaratibu wa kibepari kurudishwa kwa kila upande.

Zamani kikundi cha mahaini warivishenisti wa Soviet kilisema ya kuwa, udikteta wa kifanyakazi "umekuwa si wa lazima tena katika Soviet Union" na Soviet Union "imekuwa dola ya

watu wote".[16] Lakini sasa kinajizaba makofi kwa kusema kuwa "dola ya watu wote iendelee na jihadi ya udiktета wa kifanyakazi",[17] "dola ya watu wote" na "dola yenye udikteta wa kifanyakazi" ni "namna moja tu".[18] Vile vile walipiga makelele kwamba wataka "kutilia nguvu uongozi wa chama", "kutilia nguvu nidhamu", "kutilia nguvu ukusanyaji" na kadhalika. Mara wanasema "dola ya watu wote", mara wanasema "udikteta wa kifanyakazi", wamechanganya pamoja kwa mabavu aina mbili za mawazo yanayopingana kabisa, si kwa makusudio yo yote ila ni kwa kuwadanganya umma na kufunika udikteta wa tabaka la mabepari wakubwa tu. "Uongozi wa chama" unaokusudiwa nao ndio udhibiti wa kisiasa ufanywao na kijikundi cha maoligaki wa ufashisti wa kisoshal juu ya umati mkubwa wa wanachama wa chama na umma. "Nidhamu" inayokusudiwa nao ndiyo kuwakandamiza watu wote wa-

sioukubali utawala wao. Na "ukusanyaji" unaokusudiwa nao ndio kuyakusanya zaidi mamlaka ya kisiasa, kiuchumi na kijeshi mikononi mwa gengi lao. Kwa ufupi, wanapopeperusha vijibendera hivyo vyote, wanakusudia kutilia nguvu udikteta wa kifashisti na kujitayarisha kwa vita vya kishambulizi.

Kikundi cha mahaini warivishenisti wa Soviet ambacho kimebanwa katika taabu za nchini na ulimwenguni, kwa wazi zaidi na zaidi kinategemea nguvu za kipinga mapinduzi katika kudumisha utawala wao wa kipinga maendeleo uliomhini Lenin na Mapinduzi ya Oktoba. Katika Soviet Union ya leo, majasusi na wapelelezi wa siri wanafanya ujeuri kama watakavyo na, sheria na amri za kipinga maendeleo zinazuka bila ya kusita. Ni uhalifu kufanya mapinduzi, na kila pahala nchini watu hutiwa gerezani kwa mashtaka ya uwongo; lakini kwa wakati huo huo, upingaji

mapinduzi ni jambo la sifa na mahaini wanapongezana kwa furaha kwa vile wamepandishwa vyeo. Wanamapinduzi na watu wengi wasio na makosa yo yote wamefungwa katika kambi za wafungwa na ati "mahospitali ya wenda wazimu". Kikundi cha urivishenisti wa Soviet kimefika hadi kutuma vifaru na magari yenye deraya kuukandamiza kinyama upinzani wa umma.

Lenin aliwahi kudhihirisha: **"Hakuna sehemu yo yote duniani, ambako kunafanywa ukandamizi wa namna hii kwa sehemu kubwa ya wakaazi wake kama unavyofanywa katika Urusi"**, makabila mengine ila Warusi, yote **"yanatendewa kama ni makabila ya kigeni".**[19] Ukandamizi huo **"uliyafanya makabila yasiyo na haki za kutosha yawe na chuki nyingi na kisasi kikubwa juu ya wafalme".**[20] Sasa, matsar wepya wa urivishenisti wa Soviet wamerudisha siasa ya ukandamizi wa kikabila wa matsar wakongwe; wamechukua

hatua kali mbali mbali kama vile ubaguzi, uhamisho, mgawanyo, utiaji vizuizini kwa kuyanyonya damu na kuyatesa makabila madogo madogo na wameifanya Soviet Union kuwa **"jela ya kuwafungia umma wa makabila mbali mbali".**[21]

Kikundi cha mahaini warivishenisti wa Soviet kinatekeleza udikteta wa pande zote wa kibepari katika eneo lote la mambo ya kifikra. Nao wanaharibu na kukandamiza kiwazimu fikra na utamaduni wa kisoshalisti wa kifanyakazi; ilhali wanaachia fikra na utamaduni ulioozo kabisa wa kibepari uingie moja kwa moja kila mwahala kama mafuriko ya maji. Wanapayukwa vikubwa juu ya umilitaristi, ushovinisti wa kitaifa na ukaburu na wanachukua uandishi na sanaa kama ni vyombo vyao vya kutimizia ubeberu wa kisoshal.

Katika kuulaumu vikali utawala wa giza wa utaratibu wa kitsar, Lenin aliwahi kuainisha hivi: Ujeuri wa askari

polisi, mateso ya kinyama, na upotovu wa kimoyo umefikilia daraja ya juu kabisa ya namna hii, **"hata miamba itaguta"!**[22] Watu kama wakipenda, waweza kulinganisha kidogo utawala wa kikundi cha mahaini warivishenisti wa Soviet na utaratibu wa kitsar uliolaumiwa vikali na Lenin wakati ule.

Kutokana na upinduzi wa serikali wa kipinga mapinduzi, kikundi cha mahaini cha Khrushchov-Brezhnev kimefanya kazi ambazo ubeberu na wapinga maendeleo wote hawawezi kuzifanya. Ni kama Stalin alivyosema, **"Njia rahisi kabisa ya kuteka ngome ni kutoka ndani."**[23] Ngome ya kisoshalisti ambayo haikutekwa na uingiliaji kati wa kijeshi uliofanywa na nchi 14, uasi wa Walinzi Weupe, hujma za mamilioni ya askari wa Hitler, aina mbali mbali za uharibifu, upinduzi, mazingio na mazunguko ya ubeberu, lakini mwishowe imetekwa na kijikundi hicho cha mahaini kutoka ndani yake. Kikundi cha

Khrushchov-Brezhnev ni mahaini wakubwa kabisa katika historia ya vugu vugu la ukoministi la ulimwengu. Nao ni wahalifu wanaoshtakiwa na historia kwa uhalifu wao mkubwa unaofika mbinguni na usiosameheka.

4. USOSHALISTI MIDOMONI, UBEBERU VITENDONI

Alipowaponda mahaini wa *International* ya Pili, Lenin aliwahi kudhihirisha: Wao ni "**usoshalisti midomoni, ubeberu vitendoni, yaani uopotyunisti umegeuka kuwa ubeberu**".[24]

Kikundi cha mahaini warivishenisti wa Soviet, pia, kimeugeuza urivishenisti kuwa ubeberu wa kisoshal. Tofauti yake ni kuwa wabeberu wa kisoshal wa *International* ya Pili kama akina Kautsky hawakukamata mamlaka ya dola, waliutumikia ubeberu wa nchi zao wenyewe tu na wakachuma bahashishi ki-

dogo katika faida kubwa za kupindukia zilizonyakuliwa kutoka kwa watu wa nchi nyingine. Na ubeberu wa kisoshal wa urivishenisti wa Soviet, unawaibia na kuwatia utumwani watu wa nchi nyingine moja kwa moja kwa kutegemea mamlaka ya dola waliyoyanyakua.

Maarifa ya historia ni kwamba katika nchi ya kisoshalisti, hatamu zake za kiserikali zikinyakuliwa tu na kikundi cha urivishenisti, ama itageuzwa kuwa ubeberu wa kisoshal kama Soviet Union ilivyo, au itageuzwa kuwa nchi ya himaya au koloni kama Czechoslovakia na Jamhuri ya Watu wa Mongolia zilivyo. Sasa watu wanaweza kutambua wazi kwamba kiini cha kukamata hatamu za kiserikali kwa kikundi cha mahaini cha Khrushchov-Brezhnev ndio kuigeuza dola ya kisoshalisti iliyoundwa na Lenin na Stalin kuwa dola ya kidhalimu ya ubeberu wa kisoshal.

Kikundi cha mahaini warivishenisti wa Soviet kinabubujika tu Ulenin, uso-

shalisti na udugu wa kilimwengu wa kifanyakazi, lakini vitendoni kinafanya shughuli za uovu za ubeberu kabisa kabisa.

Midomoni kikundi cha mahaini wavishenisti wa Soviet kinasema kuwa kinatekeleza "udugu wa kilimwengu" juu ya ati "nchi za kidugu" za kwake; lakini kwa kweli hasa kimezifunga pingu baada ya pingu baadhi ya nchi za Uropa ya Mashariki na Jamhuri ya Watu wa Mongolia ndani ya sengenge za ati "ukomkubwa wa kisoshalisti" na kuzikanyaga kama kipendavyo kwa kutumia minyororo chungu nzima kama vile "Jumuia ya Mkataba wa Warsaw" na "Halmashauri ya Masaidiano ya Uchumi". Wakitumia cheo chao cha kidhalimu, wanatembeza maporojo yao ya ati "mgawiko wa kazi wa ulimwengu", "kazi maalum kwa kila nchi" na "utaratibu mzima wa uchumi", wanazilazimisha nchi hizo ziurekibishe uchumi wao wa kitaifa ufalie mahitajio ya uri-

vishenisti wa Soviet na kuzigeuza ziwe masoko ya kuuzia bidhaa zao, viwanda vya kazi ndogo ndogo vilivyo chini ya uongozi wao, mashamba ya matunda na mboga na malisho ya mifugo, ili kufanya kikatili kabisa unyonyaji damu wa kupindukia mpaka wa uchumi.

Kwa mbinu za kijeuri kabisa na za uovu kabisa, wanazidhibiti imara nchi hizo na kuweka idadi kubwa ya wanajeshi katika nchi hizo, hata wamefika hadi kwa uwazi kutuma malaki mengi ya wanajeshi kuikanyaga Czechoslovakia chini ya kwato zao za chuma na kuunda serikali ya bandia kwa singe zao. Kama matsar wakongwe waliopondwa vikali na Lenin, gengi hilo la mahaini, kabisa **"linatekeleza kanuni ya fursa maalum za kimwinyi katika kujenga mahusiano na nchi za jirani zake".**[25]

Midomoni kikundi cha mahaini wa-vishenisti wa Soviet kinanena kuwa wanazipa "msaada" nchi za Asia,

Afrika na Latin Amerika, lakini vitendoni, chini ya kisingizio cha "msaada" huo, wanajaribu kwa nguvu kuziingiza nchi kadha za sehemu hizo katika eneo lake la taathira ili kunyang'anyiana na ubeberu wa Kimarekani sehemu za katikati. Kwa njia ya kupeleka zana za kivita na rasilmali na kufanya biashara zisizokuwa za usawa, warivishenisti wa Soviet wanaiba utajiri wao wa maumbile, wanawaingilia kati katika mambo yao ya ndani na kungojea fursa kunyakua vituo vya kijeshi.

Lenin alidhihirisha: **"Katika kutekeleza siasa ya kikoloni, licha ya nia za 'zamani' zisizohesabika, rasilmali za mambo ya fedha zimeengeza nia nyingine za kupigania mahala pa kupatia nyenzo, kusafirishia rasilmali, na kunyang'anyia 'maeneo ya taathira', . . . kunyakua ardhi ya uchumi kwa jumla."**[26] Ubeberu wa kisoshal wa urivishenisti wa Soviet unakwenda

mbele kwa kufuata njia hiyo hasa ya ubeberu wa kibepari.

Midomoni kikundi cha mahaini wari-vishenisti wa Soviet kinasema kuwa "kinaunga mkono kabisa" mapigano ya kimapinduzi ya nchi mbali mbali, lakini vitendoni kinashirikiana kwa uovu na nguvu zote zipingazo kabisa maendeleo duniani ili kuharibu mapigano ya kimapinduzi ya watu wa nchi mbali mbali. Wanawatukana kiwazimu umma wa kimapinduzi wa nchi za kibepari kama ni "washenzi wa mwisho", "majambazi" na wanayafarikisha na kuyatawanya mavugu vugu ya umma katika nchi hizo. Wanatoa pesa na bunduki kwa kusaidia moja kwa moja wapinga maendeleo wa Indonesia, India na nchi nyengine kuwaua wanamapinduzi, wanafanya chini juu kuuzima moto mkali wa mapigano ya kisilaha ya watu wa Asia, Afrika na Latin Amerika na kuyakandamiza mavugu vugu ya ukom-

bozi wa kitaifa. Ni sawa sawa na ubeberu wa Kimarekani, wamejifanya kuwa askari polisi wa ulimwengu.

Midomoni kikundi cha mahaini warivishenisti wa Soviet kinasema kuwa ati kinayakubali "mapigano ya kupinga ubeberu", pengine baadhi ya wakati pia huikaripia kidogo Marekani, lakini kwa kweli hasa, kama ubeberu wa Kimarekani, wao pia ni ubeberu mkubwa kabisa ambao wanajaribu kipumbavu kuitawala dunia. Hayo ni mambo yanayotofautiana kabisa kati ya "kupinga" Marekani kwa urivishenisti wa Soviet na mapigano yafanywayo na watu wa nchi mbali mbali kwa kupinga ubeberu wa Kimarekani. Kwa ajili ya kuigawa upya dunia, urivishenisti wa Soviet na ubeberu wa Kimarekani wananyang'anyiana huku wakishirikiana kwa uovu. Vitendo vya urivishenisti wa Soviet katika mkururo wa masuala muhimu kama vile tatizo la Ujerumani, tatizo la

Mashariki ya Kati, tatizo la Asia ya Mashariki ya Kusini, tatizo la Japani na tatizo la silaha za *nuclear*, vyote ni ushahidi wa hatia zao walizozifanya katika kunyang'anyiana na kushirikiana kwa uovu na ubeberu wa Kimarekani. Wote wawili wanatekeleza siasa ya kibeberu ya kutumia nguvu na kutojali maslaha ya watu wa nchi mbali mbali. Ama ukiwepo usuluhisho wo wote baina ya urivishenisti wa Soviet na ubeberu wa Kimarekani, basi si cho chote si lote isipokuwa ni mapatano ya muda kati ya maharamia.

Lenin alidhihirisha: **"Umilitaristi wa kisasa ni tokeo la ubepari."**[27] Vita vya zama zetu **"vinatokana na tabia hasa ya ubeberu"**.[28]

Tokea Brezhnev kushika utawala, kikundi cha mahaini warivishenisti wa Soviet kinakwenda mbele zaidi na zaidi kwenye njia ya umilitaristi. Kimerithi siasa ya kistretiji ya kijeshi ya Khrush-

chov kuhusu utishiaji wa *nuclear* na kimekuza kwa nguvu silaha za *missile-nuclear*, na kwa wakati huo huo kimeengeza kwa mara mbili juhudi yake ya kupanua zana za kijeshi za kawaida, kutilia nguvu majeshi ya nchi kavu, baharini na hewani katika kila upande na kutekeleza "siasa ya manowari" ya ubeberu katika ulimwengu mzima.

Kuhusu suala la vita, zamani Khrushchov alipayukwa porojo la uhange kuhusu dunia ati "isiyo na silaha, isiyo na jeshi na isiyo na vita" ili kufunika upanuzi wa kijeshi na matayarisho ya kivita ya kweli. Na sasa, Brezhnev na washiriki wake wamebadili kidogo wimbo wao na kwa kutumia ukomo wa nguvu zao wanapandisha mori wazimu wa kivita, wanapiga makelele kuwa hali ya ulimwengu hivi sasa "imejaa hatari ya vita vipya vya dunia",[29] wanatishia kwa kusema hadharani "kumtangulia mshindani", na kujigamba ati "*missile*

za kistretiji" za kwao "zaweza kufyeka shabaha zo zote za mahala po pote".[30] Wanaengeza kwa wazimu zaidi matumizi ya mambo ya kijeshi, kuharakisha uhamasisho na matayarisho ya kufanyia vita vya kishambulizi na kupika majungu ya kuanzisha vita vya umeme wa radi vya Kihitler.

Kikundi cha mahaini warivishenisti wa Soviet kimeikalia Czechoslovakia kwa njia ya hujma za ghafla, kilishambulia ardhi ya China kama vile Kisiwa cha Chenpao na sehemu ya Tiehliekti, na kuifanyia nchi yetu matishio ya *nuclear*. Yote hayo yamefedhehesha vilivyo tabia ya ushambulizi na ujasirishaji wenye kuhatarisha wa ubeberu wa kisoshal wa urivishenisti wa Soviet. Kama ubeberu wa Kimarekani ulivyo, kijikundi cha maoligaki wa ubeberu wa kisoshal wa urivishenisti wa Soviet kimeshakuwa mhalifu mkuu mwengine akitayarisha kuanzisha vita vya dunia.

5. ULE UITWAO "UBREZHNEV" NI UDHALIMU HALISI

Kwa ajili ya kuitekeleza zaidi siasa ya ushambulizi na upanuzi ya ubeberu wa kisoshal, kikundi cha mahaini cha Brezhnev kimeukuza urivishenisti wa Khrushchov na kimeufanyiza mkururo wa "nadharia" za kifashisti zinazoitwa ati "Ubrezhnev".

Hebu, sasa tuangalie kidogo "Ubrezhnev" ni kidude gani hasa.

Kwanza, nadharia ya ati "enzi yenye mpaka". Akina Brezhnev wanasema kwamba kulinda ati "maslaha ya kisoshalisti" ya kwao ndiyo kulinda "enzi ya juu kabisa".[31] Wanatangaza hadharani kuwa urivishenisti wa Soviet una haki ya kuamua maisha ya nchi nyingine "pamoja na maisha ya enzi yao".[32]

Ati "maslaha ya kisoshalisti"! Si ye yote isipokuwa ni nyinyi ambao mmeupindua utaratibu wa kisoshalisti wa Soviet Union na kueneza msimamo wa

kirivishenisti wa kurejesha ubepari katika nchi kadha za Uropa ya Mashariki na Jamhuri ya Watu wa Mongolia. "Maslaha ya kisoshalisti" mliyoyataja ni hasa maslaha ya ubeberu wa kisoshal wa urivishenisti wa Soviet, maslaha ya ukoloni. Nyinyi mmeilazimisha "enzi ya juu kabisa" inayotawala mambo yote, juu ya watu wa nchi nyingine. Hii ndiyo kusema kwamba enzi za nchi nyingine "zina mpaka", na mamlaka yenu ya kuamrisha nchi nyingine "hayana mpaka". Hii vile vile ndiyo kusema kwamba nyinyi mna haki ya kuziamrisha nchi nyingine, lakini nchi hizo hazina haki ya kukupingeni; mna haki ya kukanyaga nchi nyingine na nchi hizo hazina haki ya kukuzuieni. Hitler aliwahi kubweka kiwazimu, ana "haki ya kuwatawala wengine".[33] Akina Dulles pia walieneza porojo la kuwa enzi ya kitaifa "imekuwa kitu kibovu",[34] na kwamba "enzi ya dola moja" yafaa kuchukuliwa mwahala pake na

ati "enzi ya muungano".[35] Kwa hivyo ni wazi kwamba porojo la Brezhnev la "enzi yenye mpaka" si cho chote kile ila ni mwangwi wa upayukwaji wa kiwazimu wa kibeberu.

Pili, nadharia ya ati "udikteta wa ulimwengu". Akina Brezhnev wametangaza kwamba wana haki ya "kukomesha matisho juu ya utaratibu wa kisoshalisti kwa kuzipelekea nchi za kidugu msaada wa kijeshi".[36] Walisema: "Lenin alibashiri" kuwa ukuaji wa kihistoria "utaugeuza udikteta wa kifanyakazi wa nchi moja kuwa udikteta wa kilimwengu ambao unaweza kutoa athari za kuamulia siasa ya dunia yote".[37]

Gengi hilo la mahaini limepotoa kabisa fikra ya Lenin.

Katika makala yaitwayo *Muswada wa Muhtasari Kuhusu Masuala ya Taifa na Koloni,* Lenin aliandika, "**kubadili udikteta wa kifanyakazi kutoka udikteta wa nchi moja (yaani uliokuwepo ka-**

tika nchi moja na usioweza kuamua siasa ya dunia nzima) kuwa udikteta wa ulimwengu (yaani udikteta wa kifanyakazi ambao kwa uchache uwepo katika nchi kadha zilizoendelea mbele na unaoweza kufanya athari za kuamua siasa ya dunia nzima)".[38] Maana hasa ya maneno ya Lenin ni kushikilia udugu wa kilimwengu wa kifanyakazi na kufanya uenezi wa siasa juu ya mapinduzi ya ulimwengu ya kifanyakazi. Lakini kikundi cha mahaini warivishenisti wa Soviet kimefika hadi kupotosha moyo wa kimapinduzi wa kifanyakazi wa kifungu hicho cha maneno ya Lenin, na kubuni porojo la ati "udikteta wa ulimwengu", na wamelichukua kama ni "hoja ya nadharia" katika kufanya uingiliaji kati wa kijeshi na ukaliaji wa kijeshi dhidi ya nchi kadha za Uropa ya Mashariki na Jamhuri ya Watu wa Mongolia. "Udikteta wa ulimwengu" mlioutaja ndio unakusudia kuzitia nchi nyingine chini ya utawala na utumwa

wa matsar wepya. Jee, kwa kutumia kisingizio cha "kusaidia nchi za kidugu" mnaweza kuionea nchi nyingine kwa nguvu zenu za kijeshi? Na, mnaweza kutuma majeshi yenu kuingia katika nchi nyingine kama mpendavyo na kufanya ujeuri huko? Chini ya bendera ya "vikosi vya muungano", mmeishambulia na kuingia katika Czechoslovakia. Jee, iko tofauti gani baina ya jambo hilo na ushambulizi wa jeshi la muungano wa nchi nane dhidi ya China katika 1900, uingiliaji kati wa kisilaha wa nchi 14 katika Soviet Union, na ushambulizi wa "nchi 16" zilizokusanywa na ubeberu wa Kimarekani dhidi ya Korea!

Tatu, nadharia ya ati "ukoo mkubwa wa kisoshalisti". Akina Brezhnev wanabubujika kwamba "ukoo mkubwa wa kisoshalisti ni kitu kizima kisichotenge-ka"[39] na ni lazima kutilia nguvu "vitendo vya pamoja"[40] vya "ukoo mkubwa wa kisoshalisti".

Ati "ukoo mkubwa wa kisoshalisti"! Hichi si cho chote si lo lote ila ni jina jingine la milki ya kikoloni, ambao nyinyi mkiwa kama dola inayoyatawala makoloni. Mahusiano baina ya nchi za kisoshalisti za kweli, kubwa au ndogo, ni lazima yajengwe juu ya msingi wa Umarx-lenin, yajengwe juu ya msingi wa kanuni za usawa kabisa, kuheshimiana ukamilifu wa nchi, kuheshimiana enzi ya dola na uhuru na kutoingiliana kati katika mambo ya ndani, na yajengwe juu ya msingi wa kanuni za kuunganana mkono na kusaidiana za udugu wa kilimwengu wa tabaka la kifanyakazi. Lakini, nyinyi mmezikanyaga nchi nyingine chini ya miguu yenu na kuzilazimisha zikubali uongozi wenu na zikutegemeeni. "Muunganisho" mliotaja unakusudia "kuziunganisha" zote pamoja siasa, uchumi, na mambo ya kijeshi ya nchi nyingine yawe mikononi mwenu. Na "kutotengeka" mlikokutaja kuna maana ya kutoruhusu nchi

nyingine zisitoke kwenye udhibiti wenu na utumwa wenu. Jee, hii siyo mnataka kuwafanya kimachomacho watu wa nchi nyingine kuwa watumwa wenu?

Nne, nadharia ya ati "mgawiko wa kazi wa ulimwengu". Akina Brezhnev wamekuza sana tena sana porojo hilo lililovumishwa na Khrushchov tangu zamani sana. Si kama wametekeleza porojo hilo la "mgawiko wa kazi wa ulimwengu" katika nchi kadha za Ulaya ya Mashariki na Jamhuri ya Watu wa Mongolia tu kama tulivyotaja juu, bali vile vile wamelieneza katika nchi za Asia, Afrika na Latin Amerika. Wanasema: Nchi za Asia, Afrika na Latin Amerika hazitaweza "kujenga uchumi wa kitaifa ulio huru" mpaka "zishirikiane" na urivishenisti wa Soviet.[41] "Kwa upande wa Soviet Union, mashirikiano hayo yameleta mayumkiniko mengi zaidi katika kutumia kwa vikubwa zaidi ubora wa mgawiko wa kazi wa ulimwengu. Kutoka nchi hizo, tuna-

weza kununua idadi kubwa ya bidhaa zao za kimila inayozidi kila kukicha kama vile pamba, sufi, ngozi ya wanyama, mawe ya madini safi yasiyo ya chuma, mafuta ya mimea, matunda, kahawa, punje za koko, chai na nyenzo nyingine pamoja na vitu vitengenezwavyo tayari."[42]

Ole "bidhaa za kimila"!

Lakini, inasikitisha, kwani orodha hii ya bidhaa haijakamilika, inapaswa iongezwe petroli, mpira, nyama, mboga, mchele, katani ya kihindi, sukari ya miwa na kadhalika.

Katika macho ya kijikundi cha maoligaki wa urivishenisti wa Soviet, watu wa nchi za Asia, Afrika na Latin Amerika wanaonekana kama wamezaliwa na wajibu huo wa kuwatolea ati "bidhaa hizo za kimila" jadi kwa jadi. "Nadharia" gani hiyo? Wakoloni na wabeberu walitangaza zamani sana kuwa wao wataamua kila nchi itoe mazao gani kwa mujibu wa hali yake ya kimaumbi-

le, na wamezilazimisha nchi za Asia, Afrika na Latin Amerika ziwe mahala pa kutoa nyenzo zao na wameziweka katika hali ya kuwa nyuma ili nchi zenye kazi za viwanda za kibepari zifanye unyonyaji damu wa kikoloni kwa urahisi kabisa na ushenzi kabisa. Kikundi cha urivishenisti wa Soviet kimerithi vilivyo siasa hiyo ya kikoloni ya ubeberu. Porojo lao la "mgawiko wa kazi wa ulimwengu" lina maana "Soviet Union ya viwanda; Asia, Afrika na Latin Amerika ya kilimo", au "Soviet Union ya viwanda; Asia, Afrika na Latin Amerika ya viwanda vya kazi ndogo ndogo viongozwavyo nao".

Madhumuni ya nchi za kisoshalisti za kweli katika kubadilishana vitu na kusaidiana na nchi za Asia, Afrika na Latin Amerika juu ya msingi wa usawa na kufaidishana, ni kwa ajili ya kuzihimiza nchi hizo zikuze uchumi wao wa kitaifa ulio huru na unaojiendesha wenyewe. Lakini madhumuni ya porojo la

"mgawiko wa kazi wa ulimwengu" linalotetewa na kijikundi cha maoligaki wa urivishenisti wa Soviet kabisa ni kwa ajili ya kufanya upenyaji, udhibiti na unyang'anyi katika nchi za Asia, Afrika na Latin Amerika na kupanua maeneo yao ya taathira na kuzifunga nchi hizo minyororo mipya ya ukoloni wa urivishenisti wa Soviet.

Tano, nadharia ya ati "kuhusika kwa maslaha yetu". Akina Brezhnev wamevumisha kwamba, "Soviet Union ambayo, ikiwa ni nchi kubwa ya dunia, inayo maingiliano ya kilimwengu yanayokuzwa kwa mapana na marefu, haiwezi kukaa kando na kuangalia tu matukio ambayo japo yako mbali nasi kwa jiografia, lakini yanahusikana na usalama wetu au wa marafiki zetu".[43] Wamefika hadi kupiga makelele kwamba "vikosi vya manowari vya Soviet" lazima "vitasafiri kwenda po pote pale ambapo panapohitajika kwa maslaha ya usalama wa nchi yetu"![44]

Jee, kwa sababu ni nchi kubwa, mnaweza kuhesabu kote duniani kuwa ni pahala penye maslaha yenu wenyewe na kunyosha mikono yenu na kufanya upanuzi katika dunia nzima? Jee, kwa sababu ya kuwa na maingiliano makubwa ya kilimwengu, mnaweza kutuma manowari zenu kwenda kila mwahala kufanya matisho na ushambulizi? Nadharia hiyo ya ati "kuhusika kwa maslaha yetu" ni porojo halisi la ubeberu juu ya siasa yao ya kishambulizi ya dunia. Wakati matsar wakongwe walipofanya upanuzi wa ardhi nchi za nje, walifanya hayo kwa kubeba bendera ya "kwa ajili ya maslaha ya Urusi". Hali kadhalika ubeberu wa Kimarekani vile vile unapiga kelele mara kwa mara, kwamba "tuna dhamana zote si kwa usalama wa peke yetu tu, bali vile vile kwa usalama wa nchi huru zote", na kwamba "tutalinda uhuru katika mahala po pote panapohitajika".[45] Usemi wa urivishenisti wa Soviet unashabihiana

kwa kiasi kikubwa kiliyoje na ule wa matsar wakongwe na wa ubeberu wa Kimarekani!

Kikundi cha mahaini warivishenisti wa Soviet ambacho kimefilisika zamani sana katika fikra, nadharia na siasa, hakiwezi kabisa kutoa cho chote kinachostahiki kutolewa, kinaweza kuokota taka taka tu kutokana na ubeberu, na baada ya kubadilisha sura yake, kikatoa nje ati "Ubrezhnev". "Ubrezhnev" huo ni ubeberu uliobandikwa alama ya "usoshalisti", udhalimu kabisa kabisa, na ni ukoloni mambo leo ulio wazi kabisa.

6. NDOTO YA URIVISHENISTI WA SOVIET JUU YA MILKI KUBWA

Kabla ya miaka mia moja iliyopita, alipoifedhehi siasa ya kishambulizi ya Urusi ya kitsar, Marx alidhihirisha: **"Njia zake, mbinu zake na hila zake**

pengine zinabadilika, lakini lengo kuu la siasa hiyo — mamlaka ya kutawala ulimwengu kwa kidhalimu halitobadilika abadan."[46]

Mfalme Tsar Nicholas wa Kwanza aliwahi kupiga kelele kwa kijeuri: "Bendera ya taifa la Urusi ikipandishwa po pote pale, lazima isishushwe tena."[47] Vizazi vingi vya matsar, wote waliwahi kuota ndoto tamu hiyo hiyo — kama alivyosema Engels — kujenga "milki kubwa ya Slav" toka Mto Elbe mpaka China, na tangu Bahari ya Adriatic mpaka Bahari ya Arctic. Hata waliwaza pia kuipanua mipaka ya milki kubwa hiyo mpaka India na Hawaii. Ili kutimiza madhumuni hayo, wao **"wanaweza kufanya uhalifu mkubwa kama wawezavyo".**[48]

Matsar wepya wa urivishenisti wa Soviet wamerithi kwa ukamilifu mila ya upanuzi wa ardhi ya matsar wakongwe na wamejichanja alama zilizokwenda ndani sana za nasaba ya Ro-

manov nyusoni mwao. Wanaota ndoto ile ile ambayo matsar wakongwe hawa-kuitimiza, na tamaa yao ya kishenzi ya kishambulizi ni kubwa zaidi tena zaidi kuliko ile ya matsar wakongwe. Urivishenisti wa Soviet umezifanya baadhi ya nchi za Uropa ya Mashariki na Jamhuri ya Watu wa Mongolia kuwa makoloni yake na nchi za himaya. Pia wanajaribu kipumbavu kuishambulia na kuikalia ardhi nyingine zaidi ya China, kwa uwazi wanafuatisha siasa ya matsar wakongwe juu ya China na kupiga kelele ya kuwa mpaka wa kaskazini wa China "ulikuweko kwenye Ukuta Mkuu".[49] Wamenyosha mikono na miguu yao katika Asia ya Mashariki ya Kusini, Mashariki ya Kati, Afrika hadi Latin Amerika, wametuma vikosi vyao vya manowari kuingia katika Bahari ya Mediterranean, Bahari ya India, Pacific na Atlantic na kujaribu kipumbavu kujenga milki kubwa ya urivishenisti wa Soviet, inayokusa-

nya Uropa, Asia, Afrika na Latin Amerika.

"Milki ya Slav" ya matsar wakongwe imetoweka kama povu zamani sana na utawala wa kitsar nafsi yake ulifyekwa na Mapinduzi Makuu ya Oktoba yaliyo-ongozwa na Lenin zamani sana katika mwaka 1917, na utawala wa matsar wakongwe ukayeyuka. Hali kadhalika, leo, katika zama hizi ambazo ubeberu unaendea kuangamia moja kwa moja itakuwa ni ndoto tu kwa matsar wepya kujaribu kipumbavu kujenga milki kubwa zaidi ya kutawala kidhalimu dunia nzima.

Stalin alisema: **"Lenin aliuita ubeberu kuwa ni 'ubepari unaokata roho'. Kwa nini? Kwa sababu ubeberu umezipeleka hitilafu za ubepari kwenye mwisho wake, kwenye kilele chake, na kupindukia hapo mapinduzi yaanza."**[50]

Maadamu urivishenisti wa Soviet umeendea njia ile ile ya ubeberu, hapana budi, unaongozwa na mwendo wa

kisheria wa ubeberu na kujitumbukiza katika mashambulio ya hitilafu za asili za aina kwa aina za ubeberu.

Komredi Mao Tsetung amedhihirisha: **"Marekani ni chui wa karatasi, msiisadiki, ikichomwa mara moja tu itatoboka. Soviet Union ya kirivishenisti pia ni chui wa karatasi."**[51]

Ilivyokuwa ubeberu wa kisoshal wa urivishenisti wa Soviet umefanya ushambulizi na upanuzi wa ardhi kwa kiwazimu, basi bila ya mwepuko wo wote utakwenda kwenye upande wake wa kinyume na kujitayarishia hali ya kuangamia kwake. Urivishenisti wa Soviet unazifanya nchi zote zilizoko katika ati "ukoo mkubwa wa kisoshalisti" kama ni ardhi zake mwenyewe, lakini kabisa hauwezi kuulazimisha kwa muda mrefu utawala wa kikoloni juu ya wananchi wa nchi hizo, wala hauwezi kulegeza mivutano yake na nchi hizo. Uropa ya Mashariki ya leo, ni kama ndoo ya baruti, ambayo hakika iko siku itaripu-

ka. Vifaru vya urivishenisti wa Soviet kuingia Prague, hakuonyeshi kabisa nguvu za ubeberu wa kisoshal wa urivishenisti wa Soviet, kinyume chake, hiyo ndiyo dalili ya kuanza kubomoka kwa milki ya ukoloni ya urivishenisti wa Soviet. Miguu iliyojaa matope ya ubeberu wa kisoshal wa urivishenisti wa Soviet imezama katika shimo lenye kina kirefu la Czechoslovakia na hawezi kuitoa mwenyewe.

Kwa upanuzi wa ardhi na unyang'anyi wake katika Asia, Afrika na Latin Amerika urivishenisti wa Soviet umejitia katika upinzani wa watu wa sehemu hizo. Umenyosha mkono wake mbali namna hii, hivyo umejitwika mzigo mkubwa, na ni kama mtu aliyevimba mwili wote. Hata magazeti ya ubeberu wa Kimarekani pia yalisema: "Tumegundua kwamba Warusi pia wamefanya kosa kubwa kama tulivyofanya sisi, ijapokuwa kosa lao si kubwa zaidi kuliko letu."[52]

Ubeberu wa kisoshal wa urivishenisti wa Soviet umejiunga katika safu la ubeberu wa ulimwengu, na hivyo umezifanya hitilafu miongoni mwa ubeberu kuwa kali zaidi. Kati yao wanafanya mapambano makali kwa ajili ya kupanua kila mmoja kwa upande wake maeneo yao ya taathira. Katika mazunguko ya duara kwa duara ya watu wa dunia, mchuano kati ya ubeberu wa kisoshal na ubeberu unaweza tu kuharakisha mwendo wa kwendea kuangamia kwa utaratibu mzima wa ubeberu.

Utawala wa ubeberu wa kisoshal wa urivishenisti wa Soviet nchini vile vile umejengeka kwenye mdomo wa volkeno. Katika siku za kipinga maendeleo za Stolypin, Lenin aliandika hivi: Mapigano ya tabaka la kifanyakazi la Urusi **"pengine yatakua kwa upesi, pengine yatakua kwa taratibu", "lakini kwa vyo vyote vile, yanakwendea kwenye mapinduzi".**[53] Leo, katika Soviet Union, mapambano na mivutano

kati ya tabaka la mabepari mabwana-serikali wenye kuhodhi la aina mpya kwa upande mmoja na tabaka la kifa-nyakazi, wakulima waishio kwa jasho lao na wataalam wa kimapinduzi walio-ko katika hali ya kitumwa kwa upande mwengine, yanakuwa makali zaidi siku hata siku. Mapigano ya kitabaka yana-kua bila ya kutegemea matakwa ya mtu na hapana budi yatasababisha mapin-duzi karibuni au baadaye.

Soviet Union hapo awali ilikuwa muungano wa dola ya kisoshalisti yenye makabila mengi. Ni katika hali ya ki-soshalisti na juu ya msingi wa usawa na kujitolea tu, ndio muungano huo wa dola yenye makabila mengi unaweza kujengwa, kuimarishwa na kukuzwa. Ni kama Stalin alivyodhihirisha: Soviet Union **"imeona maarifa ya kushindwa ya nchi za tabaka la mabepari katika kujenga dola zenye makabila mengi. Imeona maarifa ya kubomoka kwa mil-ki ya Austria-Hungary ya zamani".**

Lakini, dola ya Soviet yenye makabila mengi **"inaweza kushinda mitihani yote"**, kwani utaratibu wa kisoshalisti **"umeunda mahusiano ya ushirikiano wa kidugu wa kikweli baina ya watu wa makabila mbali mbali katika utaratibu wa umoja wa dola ya muungano".**[54] Sasa kikundi cha mahaini warivishenisti wa Soviet kimeupindua utaratibu wa kisoshalisti, kinafanya udikteta wa kibepari, kinafanya ukandamizi wa kikabila badala ya usawa wa makabila, na kufuata siasa ya kibepari ya "mwenye nguvu humla mnyonge" badala ya kusaidiana na kupendana kati ya makabila mbali mbali. Ilivyokuwa msingi wa kifanyakazi, msingi wa kisoshalisti wa muungano wa asili umetupiliwa mbali, basi, jee hautakuweko msukosuko ule ule ambao iko siku utatangazwa kubomoka kwa ati "muungano" huo mkubwa mno wenye makabila mengi unaotawaliwa na tabaka la mabepari la

aina mpya kama ilivyokuwa milki ya Austria-Hungary hapo zamani?

Kwa ajili ya kuepukana na hali ya taabani kabisa nchini na ulimwenguni, ubeberu wa kisoshal wa urivishenisti wa Soviet, kama unavyofanya ubeberu wa Kimarekani, pia unafanya kwa vikubwa matisho ya *missile-nuclear* na kuomba kupata njia ya kujiokoa kwa ujasiri wenye kuhatarisha wa kijeshi na kuanzisha kwa kiwango kikubwa vita vya kishambulizi. Lakini, jee, vita vinaweza kuufanya ubeberu na ubeberu wa kisoshal ujiokoe katika hali yao ya kukata roho? La, itakuwa kinyume chake. Historia imehakikisha bila ya kubishika kwamba vita haviwezi kabisa kuuokoa ubeberu kwenye uangamiaji wake, bali vinaweza kuuharakisha tu.

Mwenyekiti Mao anadhihirisha: **"Kuhusu suala la vita vya dunia, yako mayumkiniko mawili tu: Moja ni kuwa vita vitasababisha mapinduzi na jingine ni kuwa mapinduzi yatavizuia vita."**[55]

Mwenyekiti Mao pia anaainisha: **"Watu wa dunia nzima, unganeni na pingeni vita vya kishambulizi vianzishwavyo na ubeberu wo wote au ubeberu wa kisoshal, hususan vile ambavyo silaha zake ni mabomu ya atomik! Pindi vikitokea vita kama hivyo, watu wa dunia nzima mnapaswa kuvifyeka vita vya kishambulizi kwa vita vya kimapinduzi, na matayarisho lazima yafanywe kuanzia sasa!"**[56]

Katika elekezo hilo tukufu lililotolewa kwa mujibu wa hali ya ulimwengu ya hivi sasa, Mwenyekiti Mao ameonyesha mwelekeo wa mapigano kwa ajili ya tabaka la kifanyakazi na watu wa kimapinduzi wa dunia nzima. Inawapasa watu wa dunia nzima wadumishe hadhari kuu, wafanye matayarisho yote vyema, na wawe tayari kwa wakati wote kuwapiga pigo la kuangamiza la kithabiti washambulizi wo wote wanaothubutu kuanzisha vita!

Mnamo miaka ya karibuni, kikundi cha mahaini warivishenisti wa Soviet kikirithi mbinu zile zile za matsar wa-kongwe kimo katika kuunga mkono na kupanga nusu kwa uwazi na nusu kisiri siri ati "Vugu Vugu la Pan-Slavism" lililo jipya na kueneza ati "utukufu wa moyo wa kitaifa" wa Urusi, ili kujaribu kipumbavu kutumia miele-kezo ya mawazo hayo ya kipinga maen-deleo kuwatia sumu umma wa watu waishio kwa jasho lao na kizazi cha vi-jana wa Soviet Union na kuwashawishi kwa hila watu wa Soviet Union wajifa-nye kuwa vyombo vya kijikundi cha maoligaki wa urivishenisti wa Soviet katika kutekeleza siasa zao za kisham-bulizi na za kivita. Kwa moyo wa udhati tungependa kuwakumbusha ndugu zetu watu wa Soviet Union kwa vyo vyote wasiingie katika mtego huu wa "Pan-Slavism".

Nini "Pan-Slavism"?

Walipowafichua matsar wakongwe, Marx na Engels walidhihirisha kwa vikali kabisa: **"Pan-Slavism ni uvumbuzi wa Baraza la Mawaziri la St. Petersburg".**[57] Engels alisema: Matsar wakongwe walitumia mbinu hii ya udanganyifu katika kutayarisha vita, na **"waliifanya kuwa ni tumainio lao jembamba la mwisho katika kuuokoa utaratibu wa kitsar wa Urusi na nguvu zipingazo maendeleo za Urusi".** Kwa hivyo, **"Pan-Slavism ni adui mwovu kabisa kwetu sisi na Warusi."**[58]

Kama porojo la Hitler ati "Maaryan ni waungwana kabisa", "Pan-Slavism" ya matsar wepya wa urivishenisti wa Soviet ni ukaburu wa kipinga maendeleo kabisa. Wanaeneza fikra hizo za kipinga maendeleo, si kwa sababu yo yote ila kwa ajili ya kukitumikia kijikundi cha watawala wapingao maendeleo waliomo katika ati "makabila ya daraja ya juu" katika kupanua ardhi nchi za nje. Lakini kwa umma mkubwa

wa watu ina maana ya msiba mkubwa kabisa tu.

Lenin aliwahi kudhihirisha: **"Ukandamizi kwa 'watu wa makabila ya kigeni' ni fimbo yenye marungu mawili. Rungu moja linawapiga 'watu wa makabila ya kigeni' na jengine linalipiga kabila la Urusi."**[59] Sasa, ni hasa nyuma ya pazia la moshi la ati "Pan-Slavism", kijikundi cha maoligaki wa urivishenisti wa Soviet, kwa upande mmoja kinakazana kupanga vita vya kishambulizi na kwa upande mwengine kinaharakisha hujma zao dhidi ya watu wa Soviet Union pamoja na watu wa kabila la Urusi.

Maslaha ya tabaka la kifanyakazi na umma mkubwa wa watu wa Soviet Union yanapingana kabisa na ya matsar wepya wa urivishenisti wa Soviet, lakini yanaambatana sawasawa na maslaha ya watu wa kimapinduzi ya dunia nzima. Pindi matsar wepya wa urivishenisti wa Soviet wakianzisha kwa ki-

wango kikubwa vita vya kishambulizi, basi, kwa kufuata kanuni ya Lenin katika kupambana na vita vya kishambulizi vya ubeberu, tabaka la kifanyakazi na watu wa kimapinduzi wa Soviet Union asilan hawatokubali kuuhudumu ubeberu wa kisoshal wa urivishenisti wa Soviet katika vita visivyokuwa vya haki vitakavyoanzishwa nao. Watarithi jihadi ya wana mashujaa wa Mapinduzi Makuu ya Oktoba na kupigana kwa ajili ya kuwapindua matsar wepya na kuujenga upya udikteta wa kifanyakazi.

Kabla ya miaka mia mbili iliyopita, mtenzi mmoja wa Urusi alipompiga kilemba cha ukoka Malkia Tsarina Catherine wa Pili kwa "mafanikio" ya vita vya kishambulizi, aliandika hivi: "Songa mbele na dunia nzima itakuwa yako".[60] Sasa, matsar wepya wa urivishenisti wa Soviet wamepanda juu ya farasi wa matsar wakongwe na "kusonga mbele". Wanakimbia huko na huku wakiwa na maruirui, na wameshindwa

kuzuia hatamu, na hata wamesahau kabisa kwamba mababu wa mababu zao waliangushwa kutoka kwenye farasi huyo huyo na kumaliza milki ya Urusi katika nasaba ya Romanov. Na matsar wepya kabisa hawatokuwa na mwisho mwema zaidi kuliko ule wa matsar wakongwe, bila ya shaka wataangushwa kutoka kwenye farasi wao na kuvunjwa vipande vipande.

7. WATU WA DUNIA NZIMA, UNGANENI NA PIGANENI KWA AJILI YA KUUANGUSHA UBEBERU WA KIMAREKANI, URIVISHENISTI WA SOVIET NA WAPINGA MAENDELEO WA NCHI MBALI MBALI

Komredi Mao Tsetung alidhihirisha:

"Soviet Union ilikuwa dola ya mwanzo ya kisoshalisti na Chama cha Kikomunisti cha Soviet kilikuwa Chama kilichoundwa na Lenin. Ingawa uongozi

wa Chama na dola ya Soviet sasa umenyakuliwa na warivishenisti, lakini nawanasihi makomredi mwamini kikweli kweli kwamba umma mkubwa wa watu, umma mkubwa wa wanachama wa Chama na makada wa Soviet ni wema, ni watakao mapinduzi na kwamba utawala wa urivishenisti hautodumu muda mrefu."[61]

Watu wa China wana hisia nyingi za kirafiki juu ya watu wa Soviet Union. Katika Mapinduzi Makuu ya Oktoba yaliyoongozwa na Lenin, wafanyao kazi wa China waliokuweko Urusi walipigana bega kwa bega pamoja na tabaka la kifanyakazi la Urusi. Katika mapigano ya kimapinduzi ya muda mrefu, watu wa nchi zetu mbili wameungana mkono na kusaidiana na kuunda urafiki mkubwa. Kijikundi cha maoligaki wa urivishenisti wa Soviet kwa kiwazimu kinatia fitina na kujaribu kuharibu mahusiano baina ya watu wa nchi

mbili, China na Soviet Union, na mwisho wao utakuwa ni kulinyanyua jabali na kulibwaga miguuni mwao wenyewe.

Watu wa Soviet ni watu watukufu na wenye mila ya fahari ya kimapinduzi ambao walifunzwa na Lenin na Stalin. Wao abadan hawatovumilia kwa muda mrefu matsar wepya kukaa juu ya vichwa vyao. Ingawa matunda ya Mapinduzi ya Oktoba yamezikwa na mahaini warivishenisti wa Soviet, lakini, kanuni za Mapinduzi ya Oktoba zitadumu. Chini ya bendera kubwa ya Ulenin, mkondo wenye nguvu wa mapinduzi ya umma hakika utavunjilia mbali barafu za utawala wa urivishenisti, na *spring* ya kisoshalisti hakika itarudia tena katika ardhi kubwa ya Soviet Union!

Komredi Mao Tsetung amedhihirisha:

"Si katika China au nchi nyingine za ulimwengu, kwa ufupi, watu zaidi ya 90 kwa mia mwishowe wataunga mkono Umarx-lenin. Sasa bado wako watu

wengi duniani, ambao bado hawajazindukana kwa sababu wanadanganywa na chama cha kidemokrasi cha kisoshal, urivishenisti, ubeberu na wapinga maendeleo wa nchi mbali mbali. Lakini kwa vyo vyote vile wataamka hatua kwa hatua na kuunga mkono Umarx-lenin. Ukweli huu wa Umarx-lenin hauzuiliki. Umma wa watu hatimaye watanyanyuka katika mapinduzi. Mapinduzi ya ulimwengu hakika yatashinda."[62]

Tunapoadhimisha siku ya kutimia miaka mia tangu kuzaliwa Lenin mtukufu, tunafurahi kuona kwamba chini ya mwelekezo wa Umarx-Ulenin-Fikra Mao Tsetung, jihadi ya mapinduzi ya tabaka la kifanyakazi la ulimwengu inafululiza kupata ushindi. Nguvu za Umarx-lenin halisi za dunia nzima zinakua na kuimarika siku baada ya siku. Mapigano ya ukombozi yafanywayo na mataifa yanayokandamizwa na watu

wanaokandamizwa yanakua kimotomoto. Nchi zote na watu wote wanaoshambuliwa, kudhibitiwa, kuingiliwa kati au kuonewa na ubeberu wa Kimarekani na urivishenisti wa Soviet wamo katika kuunda muungano wa pamoja ulio mkubwa kabisa. Umeshaanza wakati mpya wa kihistoria wa kupinga ubeberu wa Kimarekani na urivishenisti wa Soviet. Kengele ya kifo cha ubeberu na ubeberu wa kisoshal inalia.

Umarx-Ulenin-Fikra Mao Tsetung isiyoshindika ni silaha yenye nguvu kubwa ya tabaka la kifanyakazi katika kuitambua na kuitengeneza dunia na ni silaha yenye nguvu kubwa ya kusukuma mbele historia. Umarx-Ulenin-Fikra Mao Tsetung ikifungamanishwa tu na mamia ya mamilioni ya umma wa kimapinduzi na matendo hasa ya mapinduzi ya watu wa nchi mbali mbali, bila ya shaka yo yote itatoa nguvu za kimapinduzi zisizomalizika na kubomo-

lea mbali dunia kongwe yote vipande vipande!

Udumu Umarx mtukufu!

Udumu Ulenin mtukufu!

Idumu Fikra Mao Tsetung iliyo tukufu!

MAELEZO

[1] "Msingi wa Ulenin", *Maandishi Yote ya Stalin*, uchapaji wa Kichina, Juzuu ya 6, uk. 63.

[2] "Programu ya Kijeshi ya Mapinduzi ya Kifanyakazi", *Maandishi Yote ya Lenin*, uchapaji wa Kichina, Juzuu ya 23, uk. 75.

[3] "Juu ya Udikteta wa Kidemokrasi wa Umma", *Maandishi Yaliyoteuliwa ya Mao Tsetung*, uchapaji wa Kichina, Juzuu ya 4, uk. 1476 na 1475.

[4] Hotuba ya Mwenyekiti Mao ya Aprili 17, 1957.

[5] "Ubeberu na Mafarikiano ya Usosha-listi", *Maandishi Yote ya Lenin*, uchapaji wa Kichina, Juzuu ya 23, uk. 117.

[6] "Dola na Mapinduzi", *Maandishi Yaliyoteuliwa ya Lenin*, uchapaji wa Kichina, Juzuu ya 3, uk. 179.

[7] Kama juu, uk. 184.

[8] "Mapinduzi ya Usoshalisti na Haki ya Mataifa Juu ya Kujiamulia Wenyewe", *Maandishi Yote ya Lenin*, uchapaji wa Kichina, Juzuu ya 22, uk. 138.

[9] "Mapinduzi ya Kifanyakazi na Haini Kautsky", *Maandishi Yote ya Lenin*, uchapaji wa Kichina, Juzuu ya 28, uk. 235.

[10] "Dola na Mapinduzi", *Maandishi Yaliyoteuliwa ya Lenin*, uchapaji wa Kichina, Juzuu ya 3, uk. 192.

[11] Hotuba ya Mwenyekiti Mao katika Mkutano wa Pili wa Wanakamiti Wote wa Kamiti Kuu ya Nane ya Chama cha Kikoministi cha China, Novemba 15, 1956.

[12] Hotuba ya Mwenyekiti Mao katika Mkutano wa Kazi wa Kamiti Kuu wa Peitaiho mnamo Agosti 1962 na ya Mkutano wa Kumi wa Wanakamiti Wote wa Kamiti Kuu ya Nane ya Chama mnamo Septemba mwaka huo huo.

[13] *Ilani* ya Kamiti Kuu ya Chama cha Kikoministi cha China, Mei 16, 1966.

[14] Mazungumzo ya Mwenyekiti Mao mnamo Agosti 1964.

[15] Mazungumzo ya Mwenyekiti Mao mnamo Mei 11, 1964.

[16] *Programu ya Chama cha Kikoministi cha Soviet Union*, ilipasishwa katika "Mkutano Mkuu wa 22" wa urivishenisti wa Soviet.

[17] *Muhtasari wa Uadhimisho wa Mwaka wa Mia Tokea Kuzaliwa Vladimir Ilyich Lenin* wa urivishenisti wa Soviet.

[18] Gazeti la *Pravda* la urivishenisti wa Soviet, Machi 5, 1970.

[19] "Usoshalisti na Vita", *Maandishi Yote ya Lenin*, uchapaji wa Kichina, Juzuu ya 21, uk. 285.

[20] "Hotuba Katika Mkutano Mkuu wa Kwanza wa Wajumbe wa Jeshi la Baharini la Urusi Nzima", *Maandishi Yote ya Lenin*, uchapaji wa Kichina, Juzuu ya 26, uk. 322.

[21] "Tabaka la Kifanyakazi la Kimapinduzi na Haki ya Mataifa Juu ya Kujiamulia Wenyewe", *Maandishi Yote ya Lenin*, uchapaji wa Kichina, Juzuu ya 21, uk. 392.

[22] "Maelezo ya Mambo ya Ndani", *Maandishi Yote ya Lenin*, uchapaji wa Kichina, Juzuu ya 5, uk. 258.

[23] *Kitabu cha Masomo Mafupi cha Historia cha Chama cha Kikoministi cha Soviet Union (Bolshevik)*, uchapaji wa Ki-

china, kilipigwa chapa na Jumba la Uchapaji la Umma, uk. 471.

[24] "Juu ya Kazi za *International* ya Tatu", *Maandishi Yote ya Lenin*, uchapaji wa Kichina, Juzuu ya 29, uk. 458.

[25] "Juu ya Ufahari wa Kitaifa wa Warusi Watukufu", *Maandishi Yote ya Lenin*, uchapaji wa Kichina, Juzuu ya 21, uk. 85.

[26] "Ubeberu ni Daraja ya Juu Kabisa ya Ubepari", *Maandishi Yote ya Lenin*, uchapaji wa Kichina, Juzuu ya 22, uk. 293.

[27] "Umilitaristi Utakao Sana Vita na Mbinu za Chama cha Kidemokrasi cha Kisoshal Zipingazo Umilitaristi", *Maandishi Yote ya Lenin*, uchapaji wa Kichina, Juzuu ya 15, uk. 166.

[28] "Mkutano Mkuu wa Nane wa Wajumbe wa Chama cha Kikoministi cha Urusi (Bolshevik)", *Maandishi Yote ya Lenin*, uchapaji wa Kichina, Juzuu ya 29, uk. 168.

[29] Gazeti la *Uchitelskaya* la urivishenisti wa Soviet, Februari 5, 1970.

[30] Makala ya A.A. Grechko, Waziri wa Ulinzi wa Nchi wa urivishenisti wa Soviet. Tazama Gazeti la *Wakoministi* la urivishenisti wa Soviet, toleo la 3, 1969.

[31] Gazeti la *International Affairs* la urivishenisti wa Soviet, toleo la 11, 1968.

[32] Gazeti la *Krasnaya Zvezda* la urivishenisti wa Soviet, Februari 14, 1969.

[33] Tazama *Hukumu ya Nuremberg*, Juzuu ya 2.

[34] Tazama *Foreign Affairs*, gazeti la Marekani, Oktoba 1957.

[35] P.C. Jessup, *Sheria ya Ulimwengu ya Kisasa.*

[36] Hotuba ya L.I. Brezhnev katika "Mkutano Mkuu wa 5" wa urivishenisti wa Poland, Novemba 12, 1968.

[37] Ripoti ya K.T. Mazurov kwenye "Mkutano wa Sherehe" ya Sikukuu ya Mapinduzi ya Oktoba katika Moscow, Novemba 6, 1968.

[38] "Muswada wa Muhtasari Kuhusu Masuala ya Taifa na Koloni", *Maandishi Yaliyoteuliwa ya Lenin*, uchapaji wa Kichina, Juzuu ya 4, uk. 292.

[39] Gazeti la *Izvestia* la urivishenisti wa Soviet, Julai 2, 1968.

[40] *Waraka wa Msingi* wa Mkutano Muovu wa Moscow wa Juni, 1969.

[41] Hotuba ya L.I. Brezhnev katika Mkutano Muovu wa Moscow, Juni 7, 1969.

[42] Ripoti ya A.N. Kosygin katika "Mkutano Mkuu wa 23" wa urivishenisti wa Soviet, Aprili 5, 1966.

[43] Ripoti ya A.A. Gromyko katika "Mkutano wa Juu Kabisa wa Soviet", Julai 10, 1969.

[44] Hotuba ya S.G. Gorshkov, Amri Jeshi Mkuu wa Jeshi la Baharini la urivishenisti wa Soviet katika Sikukuu ya Jeshi la Baharini la Soviet Union mnamo mwaka 1969.

[45] Hotuba ya Rais wa Zamani wa Marekani Johnson, Juni 3 na 20, 1964.

[46] Marx, "Hotuba Kwenye Mkutano wa Uadhimisho wa Mwinuko wa Poland Katika London Mnamo Januari 22, 1867", *Maandishi Yote ya Marx na Engels*, uchapaji wa Kichina, Juzuu ya 16, uk. 226.

[47] G.I. Nevelskoi, *Michango ya Maofisa wa Jeshi la Baharini la Urusi Katika Mashariki ya Mbali ya Urusi*, uk. 124.

[48] Engels, "Siasa ya Nchi za Nje ya Serikali ya Kitsar ya Urusi", *Maandishi Yote ya Marx na Engels*, uchapaji wa Kichina, Juzuu ya 22, uk. 17.

[49] "Taarifa ya Serikali ya Soviet Union" ya Juni 13, 1969.

[50] "Msingi wa Ulenin", *Maandishi Yote ya Stalin*, uchapaji wa Kichina, Juzuu ya 6, uk. 65.

[51] Mazungumzo ya Mwenyekiti Mao ya Januari 30, 1964.

[52] *Habari za Marekani na Ripoti ya Dunia*, Januari 5, 1970.

[53] "Kuanza Kwa Maandamano", *Maandishi Yote ya Lenin*, uchapaji wa Kichina, Juzuu ya 16, uk. 357.

[54] Stalin, "Kuhusu Muswada wa Katiba ya Soviet Union", *Masuala ya Ulenin*, uchapaji wa Kichina, kilipigwa chapa na Jumba la Uchapaji la Umma mnamo mwaka 1964, uk. 649-650.

[55] Komredi Lin Piao, *Ripoti Katika Mkutano Mkuu wa Tisa wa Kitaifa wa Wajumbe wa Chama cha Kikoministi cha China.*

[56] *Kuikaribisha Miaka ya Kumi la Saba Iliyo Mikubwa* — Makala ya Wahariri wa Magazeti ya *Renmin Ribao, Hongqi* na *Jiefangjun Bao* ya Mwaka Mpya 1970. *Renmin Ribao*, Januari mosi, 1970.

[57] Marx na Engels, "Muungano wa Kidemokrasi wa Kisoshalisti na Jumuia ya Wafanyakazi ya Kilimwengu", *Maandishi Yote ya Marx na Engels*, uchapaji wa Kichina, Juzuu ya 18, uk. 492.

[58] Engels, Barua Kwa Karl Kautsky Mnamo Februari 7, 1882, *Marx na Engels Juu ya Sanaa*, uchapaji wa Kichina, kilipigwa chapa na Jumba la Uchapaji la

Uandishi wa Umma mnamo mwaka 1963, Kitabu cha 3, uk. 361.

[59] "Usawa wa Kitaifa", *Maandishi Yote ya Lenin*, uchapaji wa Kichina, Juzuu ya 20, uk. 233.

[60] G.R. Dershavin, *Kwa Ajili ya Kuiteka Warsaw.*

[61] Hotuba ya Mwenyekiti Mao katika Mkutano wa Kazi Uliopanuliwa wa Kamiti Kuu ya Chama cha Kikoministi cha China, Januari 30, 1962.

[62] Kama juu.